

**SHULE YA UPIILI YA ALLAINCE
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA
2016**

KISWAHILI KIDATO CHA PILI.

Muda: Saa 2 ½

Jibu Maswali yote.

Majibu yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa Matumizi ya Mtahini pekee.

SEHEMU	UPEO	TUZO
A. INSHA	20	
B. MATUMIZI YA LUGHA	50	
C. ISIMU-JAMII	10	
D. FASIHI SIMULIZI	20	
JUMLA		

SEHEMU A: INSHA (ALAMA 20)

Wewe ni mkuu wa Elimu Katika gatuzi lako. Andika hotuba utakayotoa katika warsha ya washikadau wa sekta ya elimu kuhusu sababu zinazowafanya vijana wengi kuacha shule.

SEHEMU B: MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 50)

a) Irabu zifuatazo hutamkwa ulimi ukiwa na mkaof gani kinywani?

- | | | |
|------|-----------|---------|
| i) | /i/ _____ | alama ½ |
| ii) | /u/ _____ | alama ½ |
| iii) | /e/ _____ | alama ½ |
| iv) | /o/ _____ | alama ½ |
| v) | /a/ _____ | alama ½ |

b) Taja sifa zozote tano za lugha

- | | | |
|------|-------|---------|
| i) | _____ | alama 1 |
| ii) | _____ | alama 1 |
| iii) | _____ | alama 1 |
| iv) | _____ | alama 1 |
| vi) | _____ | alama 1 |

c) Tofautisha kati ya:

- | | | |
|-------|-----------------------|---------|
| i) | Maimuna alinikimbilia | alama 1 |
| <hr/> | | |
| ii) | Maimuna alinikimbia | alama 1 |

d) Eleza kwa kutoa mifano matumizi mawili ya kiambishi maalmu "KU"

- | | | |
|------|-------|---------|
| (i) | _____ | alama 1 |
| (ii) | _____ | alama 1 |

e) Andika sentensi zifuatazo kwa wingi:

- | | | |
|-------|--|-----------|
| (i) | Gari lile linafuka moshi kwa vile limeharibika. | (alama 1) |
| <hr/> | | |
| (ii) | Ni dirisha lipi lililofungwa na wewe nilipolala? | (alama 1) |

- f) Tumia viunganishi vifuatavyo katika sentensi.
 (i) Fauka ya _____
 (ii) Minghairi ya _____ (alama 2)
- g) Andika visawe vya kila mojawapo ya maneno haya;
 (i) Heshima _____
 (ii) Idhini _____ (alama 2)
- h) Eleza maana ya misemo ifuatayo:
 (i) Kula mlungula _____
 (ii) Enda arijojo _____
- i) Tunga sentensi ukitumia neno "lile" kama:
 (i) Kivumishi _____
 (ii) Kiwakilishi _____ (alama 2)
- j) Tunga sentensi kuonyesha unajua tofauti kati ya maneno yafuatayo:
 (i) Nta _____
 (ii) Ncha _____ (alama 2)
- k) Tumia -enye au -enyewe kukamilisha sentensi zifuatazo:
 (i) Wanafunzi _____ shida husaidiwa
 (ii) Wanafunzi _____ walicheza vizuri (alama 2)
- l) Andika sentensi inayoonyesha ki ya masharti. (alama 1)

Tunga Sentensi kubainisha maana mbili za vitawe hivi. (alama 4)

- (i) Nyoka _____

 (ii) Hema _____

Ainisha maneno katika sentensi ifuatayo:

Mwalimu yule mzuri alikuwa anatuzwa leo.

(alama 3)

Tofautisha sentensi zifuatazo

Kamau amemwagia Njoroge uji

(alama 2)

Kamau na Njoroge wamemwagiana uji.

(alama 2)

Fuata maagizo

(i) Jaza pengo kwa neno lenye asili moja na kitenzi kilichopigwa mstari

Atur anamiliki magari na majumba mengi;

Hii ardhi yote ni _____ yake.

(alama 2)

(ii) Jaza pengo kwa kielezi mwafaka kutokana na nomino iliyopigwa mstari. (alama 2)

Hassan anamiliki shule kubwa. Leo hafiki _____

Sahihisha sentensi hii kwa njia mbili

(alama 4)

Dereva ambaye aendeshaye kwa uangalifu husamilika

Taja mbinu iliyotumika katika sentensi hii: Baada ya kumuwait alienda home amesikitika

(alama 1)

Andika methali yenye maana kunyume na ifuatayo:

Mwenye pupa hadiriki kula tamu.

(alama 1)

